

## **A Jaribio la Imani.**

- ❖ Mungu hajawahi kuomba kafara ya mwanadamu (Yer. 7:31). Mbaya zaidi, kumtoa kafara Isaka kulienda kinyume na ahadi: “kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa.” (Mwz. 21:12) Je, Ibrahimu hakulielewa agizo la Mungu (Mwz. 22:2)?
- ❖ Mungu alikuwa akimjaribu Ibrahimu. Moyo wake ulihukumiwa (Kumb. 8:2). Matokeo yalilidhisha (Mwz. 22:12)

## **B Kutimizwa kwa ahadi.**

- ❖ Isaka aligundua kuwa hapakuwa na mnyama wa kafara. Ibrahimu aliyarka maswali ya Isaka kwa kusema kuwa Mungu atajipatia.
- ❖ Kwa kweli, Mungu alijipatia mnyama kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa. Mnyama huyo alikuwa kwa niaba ya Isaka (Mwz. 22:13). Mungu akathibitisha kutimizwa kwa ahadi kwa namna hii (Mwz. 22:18).
- ❖ Mungu ametoa. Yesu ni mwana kondoo aliyekufa ili tuishi (Yn. 1:36; Rum. 5:8; 6:8).

## **C Kuchukua umiliki wa nchi.**

- ❖ Ibrahimu “alikuwa na umri wa miaka mia na ishirini” (E.G.W., PP 147) pale Mungu alipomwambia amtoe Isaka kafara. Kwahiyo, Isaka alikuwa na miaka 20, na Sara alikuwa na miaka 110.
- ❖ Miaka 17 badae, Sara alikufa (Mwz. 23:1). Ndiye mwanamke pekee katika Agano la Kale ambaye wakati wa kufa umri wake unatajwa. Lakini pia alikuwa mwanamke wa kwanza kuingia katika nchi ya ahadi.
- ❖ Baada ya kujadiliana na Efroni, Ibrahimu alinunua shamba lake la kwanza ambalo angeliita kuwa la kwake katika Kanaani (Mwz. 23:17-18).

## **D Kumpata mzao.**

- ❖ Ibrahimu alifanya mpangi kumtafutia Isaka mke ili kulinda uzao wake (Mwz. 24:1-4).
- ❖ Kuna vielelezo viwili maarufu katika kisa hiki: ombi [la Ibrahim, la Eliezeri, la Isaka], na kuamini kuwa Mungu mwongozaji wa hatua hiyo.
- ❖ Hata hivyo, Mungu alimwacha Rebeka achague mwenyewe (Mwz. 24:8, 50-51, 57-59).

## **E Wazao zaidi wa Ibrania.**

- ❖ Ibrahimu aliishi miaka 175 (Mwz. 25:7). Kando na Isaka, alikuwa na mtoto 1 na Hagari (Mwz. 25:12), na wengine 6 na Keturah (Mwz. 25:1-2).
- ❖ Ibrahimu aliwapeleka wanae saba wa masuria wake mbali kwasababu ni Isaka tu alikuwa mrithi wa nchi ya ahadi (Mwz. 25:6).
- ❖ Kuna kumbukumbu ya vizazi viwili katika Mwanzo 25:2-4 na 12-18 ambavyo vinasisitiza kuwa ahadi kwa Ibrahimu ilitimizwa: “nawe utakuwa baba wa mataifa mengi.” (Mwz. 17:4)
- ❖ Bwana alibakia kuwa mweli kwa ahadi zake kwa mtumishi Wake mwaminifu Ibrahimu, ambaye imani yake imeonyeshwa katika Maandiko kama mfano mkuu wa wokovu kwa imani.